

»Jinsi ya kuanzisha ufugaji wa ng'ombe maziwa na kuufanya uwe mradi wenyе faida – Embori sehemu ya 2«

Baada ya kukamua ng'ombe kwa kutumia mashine tumbukiza kifaa cha kukamulia kwenye ndoo iliyo na dawa ya mastrite, ambayo hufanya kama iodini. Kabla ya kupaka dawa kwenye matiti ya ng'ombe hakikisha kwamba hatakurushia mateke, na kisha chovya matiti kwenye kikombe kilicho na dawa.

Bonyeza kikombe sehemu ya chini ili kupandisha dawa juu na utumbukize matiti kwenye dawa.

Usimamizi wa ndama

Usimamizi wa ndama huanza kabla ya hawajazaliwa hadi kuachishwa kunyonya.

Mafunzo ya usimamizi wa ndama yanapaswa kutolewa kwa wafugaji ili kupunguza athari mbaya za uzazi, na ndama kuzaliwa wamekufa.

Kuzaliwa kwa ndama

Weka kumbukumbu sahihi na ufuatilie ng'ombe mara nyingi zaidi wakati wanapokaribia kuzaa.

Ndama anaweza kuzaliwa wakati miguu ya mbele inatoka wanze kisha kichwa. Pia, anaweza kuzaliwa wakati miguu ya nyuma inatoka kwanza.

Ng'ombe huhitaji msaada iwapo atachelewa kuzaa zaidi ya masaa 5.

Kulisha ndama

Ndama anapaswa kunyonya kutoka kwa mama angalau siku tatu, kisha tenganisha ng'ombe kulingana na umri na anza kuwalisha maziwa kwa njia bandia.

Maziwa yanaweza kutolewe kwa kutumia chupa au ndoo.

Kati ya wiki 2 hadi 3 za umri walishewa chakula cha wishwa, na pia wape chakula cha nyongeza. Unapotumia nyasi hakikisha kuwa ni za ubora wa juu, laini na zimechanganywa na kunde.

Mafunzo ya kibinagsi

Ndama hula hadi asilimia 10% ya uzito wa mwili wake kwa takriban wiki 6.

Kujihusisha na mbinu ya kujifunzia kupitia miradi ya mafunzo ya televisheni, hadithi za ukulima za kila siku katika magazeti na makala za mtandaoni ili kuboresha uzalishaji.